INTERNATIONAL BACCALAUREATE
BACCALAURÉAT INTERNATIONAL
BACHILLERATO INTERNACIONAL

N00/251/S(1)T

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHELI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Wednesday 8 November 2000 (afternoon)
Mercredi 8 novembre 2000 (après-midi)
Miércoles 8 de noviembre del 2000 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1 (Text handling).
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir ce livret avant d’y être autorisé.
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1 (Lecture interactive).
- Répondre à toutes les questions dans le livret de questions et réponses.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos requeridos para la Prueba 1 (Manejo y comprensión de textos).
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# UTABIRI WA ISHARA

**Na Philip Kajura**

**Kifungu cha kwanza**

KAMA leo utaamua kumvizia mtu kwa nia ya kukorofishana naye kinyota hali hii inatafsiri kuwa kuna bahati ya kifedha itakayokutokea lakini baadaye kuyeyuka, hasa wewe ambaye nyota yako ni Mbuzi (Capricorn), Samaki (Pisces), Ng'ombe (Taurus), Simba (Leo), Mashuke (Virgo) na Nge (Scorpio).

**Kifungu cha pili**

Hamu ya kuonana na umpendaye ikiongezeka leo, hii inatafsiri kuwa unapenda kuwatendea watu haki, hasa wewe ambaye nyota yako ni Simba (Leo), Mizani (Libra), Mshale (Sagittarius), Ndoo (Aquarius), Kondoo (Aries) na Mapacha (Gemini).

**Kifungu cha tatu**

Iwapo utasimamishwa kazi leo, hali hii inatafsiri kuwa uwe mwangalifu kuhusu ajali, hasa za barabarani wewe ambaye nyota yako ni Kaa (Cancer), Mashuke (Virgo), Mizani (Libra), Nge (Scorpio), Mbuzi (Capricorn) na Kondoo (Aries).

**Kifungu cha nne**

Ukipiga simu leo ikakatika kabla hujampata unayemhitaji, hali hii inaashiria kuwa unao marafiki lakini wasio na faida kubwa kwako kwa sasa, hasa wewe ambaye nyota yako ni Mizani (Libra), Nge (Scorpio), Mshale (Sagittarius), Samaki (Pisces), Mapacha (Gemini), Kaa (Cancer) na Simba (Leo).

**Kifungu cha tano**

Kama utapoteza anwani muhimu leo, hali hii inatafsiri kuwa kuna wanaokukorofisha kwa faida yao, hasa wewe ambaye nyota yako ni Ndoo (Aquarius), Kondoo (Aries), Ng'ombe (Taurus), Simba (Leo), Nge (Scorpio) na Mshale (Sagittarius).

**Kifungu cha sita**

Kama leo utanunua nyama ya porini, hali hii inatafsiri kuwa unatakiwa kufanya kafara haraka kabla mwaka huu haujaisha hasa wewe ambaye nyota yako ni Samaki (Pisces), Kondoo (Aries), Mapacha (Gemini), Kaa (Cancer), Mashuke (Virgo) na Mshale (Sagittarius).

**Kifungu cha saba**

Kama leo utapokea barua kutoka kwa rafiki yako muhimu hali hii inatafsiri kuwa kuna mipango yako itakayozaa matunda mazuri kipindi kisicho kirefu kutoka leo hasa wewe ambaye nyota yako ni Kondoo (Aries), Ng'ombe (Taurus), Kaa (Cancer), Simba (Leo), Mshale (Sagittarius), Mbuzi (Capricorn) na Samaki (Pisces).

**Kifungu cha nane**

Pesa ikikupiga chenga sana na kukupa wingi wa fikra, hali hii inatafsiri kuwa nyota yako si nzuri, hivyo unatakiwa kupata ushauri juu ya maisha hasa wewe ambaye nyota yako ni Mbuzi (Capricorn), Ndoo (Aquarius), Ng'ombe (Taurus), Simba (Leo), Mizani (Libra), Nge (Scorpio) na Mshale (Sagittarius).

**Kifungu cha tisa**

Kama itatokea leo ahadi uliyoahidiwa ukagundua kuwa kumbe ilikuwa ya uongo, hali hii kinyota inatafsiri kuwa pale unapoishi kwa sasa kuna mushikeli, hasa wewe ambaye nyota yako ni Simba (Leo), Mashuke (Virgo), Nge (Scorpio), Mbuzi (Capricorn), Ndoo (Aquarius) na Kaa (Cancer).

**Kifungu cha kumi**

Iwapo leo utapiga redio kwa kelele na kulalamikiwa, hali hii inatafsiri kuwa baadhi ya rafiki zako ni waongo, hasa wewe ambaye nyota yako ni Mbuzi (Capricorn), Samaki (Pisces), Kondoo (Aries), Mapacha (Gemini), Simba (Leo), Mizani (Libra) na Nge (Scorpio).

**KIFUNGU B**

# Utunzaji wa ngozi

❶ NGOZI huukinga mwili dhidi ya athari za kimazingira na wengi wetu huwa tunalichukulia suala la utunzaji ngozi kijuujuu tu. Watu hawatambui kwamba kutunza ngozi ni muhimu kama ilivyo kusafisha meno. Ngozi isipotunzwa vizuri hukauka, hupasuka, hubanduka, huwasha na hata kuvimba.

❷ Uharibifu huo wa ngozi ulioelezwa huweza kuruhusu ngozi kupata maambukizi kutokana na vijidudu kama bakteria na virusi. Utunzaji wa ngozi ni lazima uanze tangu mtoto anapozaliwa na kuendelea maisha yake yote.

❸ Kila binadamu ana mafuta ya asili katika ngozi yake. Mafuta hayo huitwa *sebum* na hutengenezwa na tezi (glands) zilizoko kwenye ngozi. Wakati mafuta hayo yanapoondolewa na matumizi ya mara kwa mara ya vitu kama sabuni, ngozi hukauka na kupelekea kupasuka na kubanduka. Ngozi inapopasuka huwasha, kuvimba na kuchoma choma.

❹ Kwa kawaida, vitu vinavyosababisha ngozi kukauka ni pamoja na sabuni, kuoga maji ya moto sana, au kuoga kwa muda mrefu na kuoga mara kwa mra. Watu wengi husafisha ngozi zao kupita kiasi.

**Usafishaji wa ngozi kwa kila siku (dakika 15-20 kwa siku).**

❺ Kila siku unapooga, jaribu kutumia maji ya uvuguvugu. Maji ya moto hukausha unyevunyevu uliopo kwenye ngozi. Jaribu kufupisha muda wa kuoga kwa kutumia dakika zisizozidi 15. Kuoga mara kwa mara husababisha mafuta ya asili kuondolewa katika mwili na hivyo ngozi kukauka.

❻ Epuka kutumia sabuni za kufulia ambazo zina kemikali nyingi (harsh soap). Ni mara chache sabuni za kuogea hukausha ngozi. Hata hivyo *skin cleansers* kama vile *toner* ni nzuri zaidi kwa kulainisha ngozi kuliko hata sabuni za kuogea.

❼ Tumia sabuni zaidi katika sehemu zinazotoa harufu mbaya kama makwapa, sehemu za siri na miguuni kuliko sehemu nyingine za mwili.

❽ Unapojikausha mwili baada ya kuoga usisugue ngozi, kausha kiasi cha kubakisha unyevunyevu kwenye ngozi.

❾ Baada ya hapo paka mafuta ya kulainisha ngozi kama *Petroleum jelly, jelly cream au lotion*. Zingatia zaidi sehemu za mwili zinazokauka. *Petroleum jelly* ni nzuri zaidi kwa ngozi iliyokauka sana na *lotion* inafaa kama ngozi yako ina mafuta ya asili ya kutosha unaweza kuacha kutumia mafuta ya *lotion*.

❿ Sehemu zote zinazopigwa na jua kama uso, masikio, mikono na nyuma ya shingo ni lazima zipakwe losheni au malai kila siku.

⓫ Namna ya kusafisha ngozi ya kichwa na nywele (dakika tano hadi 10 kila siku).

⓬ Vinyweleo vilivyoota kwenye ngozi hasa kichwani, huwa na tabia ya kugandamiza chembe chembe za ngozi zilizokufa. Chembe chembe hizo zinapolundikana, hutoka nje ya ngozi na kupukutika. Chembe hizo huitwa mba.

⓭ Mba waweza kuepukwa au kupungua endapo mtu atatumia *shampoo* kuoshea nywele zake walau mara mbili kwa wiki.

⓮ Kusugua nywele na ngozi ya kichwa chako kwa kutumia ncha za vidole vyako ni muhimu kwa ajili ya kuondoa mafuta na uchafu.

⓯ Tumia maji ya baridi kabla na baada ya kupaka *shampoo* siku zote. Maji ya moto hufanya nywele zako kuonekana hazina nguvu au kuwa laini kupita kiasi.

⓰ Tumia *shampoo* utakayoipendelea.

**Tahadhari:**


* ***[–Mfano–]*** ya wataalam wanaamini [–32–] kukaa [–33–] muda mrefu juani hasa katika miaka 18 ya mwanzo [–34–] uhai wako, kunaweza kukusababishia kupata kansa ya ngozi. [–35–] unawafundisha watoto wako madhara ya jua.

* Mwanga wa jua husababisha kansa, ngozi [–36–] na kupata makunyanzi. Hakuna kitu muhimu katika kutunza ngozi yako kama [–37–] na mionzi mikali ya jua.

* Unashauriwa kutumia *shampoo* za aina mbalimbali ili kuondoa [–38–] yaliyoachwa na aina nyingine ya *shampoo*.

**KIFUNGU C**

# Mgonjwa kikongwe aomba *‘Ze Gongo’* Hospitali




HAKUNA aliyeweza kuamini hata wagonjwa wenzake walibaki midomo wazi pale mgonjwa mmoja kikongwe wa miaka 65 alipoomba aletewe kilevi cha aina ya Gongo huku akiwa mahututi wodini.

Tukio hilo lililoshuhudiwa na mtoa habari wetu wa karibu aliyekuwamo wodini humo alilieleza gazeti hili kuwa, hatua hiyo ilifikiwa baada ya mgonjwa huyo kupewa chaguo la nini aletewe kutoka nyumbani kwake.

Kikongwe huyo ambaye ni Mpale wa kutoka Same, alikuwa amelazwa katika hospitali moja iliyopo mjini Moshi, ambamo alikuwamo hospitalini humo akisumbuliwa na ugonjwa wa Kisukari.

Hatua hiyo iliwashangaza wagonjwa wenzake wodini humo, wagonjwa walimshuhudia mzee huyo (jina tunalo) akiwa na chupa ya chai ambamo ndani yake ndimo mulikuwa na pombe hiyo ya Gongo.

Hakuna hata mmoja aliyekuwa akijua kuwa mgonjwa huyo alikuwa akimimina chai katika kikombe, lakini kinyume cha matazamio ya wengi kikongwe huyo alionekana kukunja uso, hatua ambayo ilipelekea wagonjwa wenzake kumuuliza kulikoni.

“Tulimuona akikunja uso wake mara alipokuwa akinywa chai hiyo, lakini tulipokwenda karibu na kuchukuwa kile kikombe ndipo tukagundua kuwa ile aliyokuwa akinywa haikuwa chai bali ni pombe ya gongo” alizungumza mtoa habari wetu alipokuwa akimsimulia mwandishi wa habari hizi.

Hatua hiyo iliripotiwa kwa mganga wa zamu wa wodi hiyo, hakukuwa na hatua yoyote aliyochukuliwa mgonjwa huyo kwa madai kuwa pengine pombe hiyo ingemsaidia kupata nafuu kiakili,…… Mambo hayo.